t

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR.BATILDA BURIAN**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE ZA SERIKALI TANZANIA

## SEKONDARI YA WASICHANA DR. BATILDA BURIAN

**Des 2025**

**KALIUA**

**TABORA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR. BATILDA BURIAN**


**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule**

**0719976828/0754280985**

**Makamu Mkuu wa shule**
**0759791765/0675302540**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR.BATILDA BURIAN,**
**S.L.P 56,**
**TABORA.**
**Tarehe 5/12/2025**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR.BATILDA BURIAN, HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA MKOA WA TABORA MWAKA 2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule hii mwaka **2026.**

Shule ya **Sekondari ya DR.BATILDA BURIAN** ipo Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kata ya Igagala kijiji cha Wachawaseme, Magharibi mwa kituo cha mabasi cha Kaliua na stesheni ya reli, umbali wa Kilometa thelathini na nane (38) kutoka stesheni ya reli na kilomita thelathini na sita (36) kutoka kituo cha mabasi cha Kaliua kuelekea Kigoma. Shule imepakana na barabara kuu ya lami inayotoka mjini Kaliua kwenda mkoa wa Kigoma, upande wa kusini. Kutoka stesheni au kituo cha mabasi unapanda mabasi/Noah/Coaster zinazokwenda Usinge au Kigoma, utashuka kijiji cha Wachawaseme/Igagala namba tisa (sekondari ya wasichana). Nauli elfu nne (4000/=).

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13/01/2026, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 09/01/2026, Mwisho wa kuripoti ni tarehe 23/01/2026.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule(Darasani)

i. Sketi ya shule ni draft (angalia sampuli ya kitambaa kwenye fomu hii).Kwa Maelezo ya mshono NI RINDA BOX (MBELE NA NYUMA) NA MARINDA MATATU KULIA NA MATATU KUSHOTO, urefu ifike kwenye kifundo cha miguu .

ii. Aje na mashati 02 meupe yenye mikono mifupi yenye ukosi wa kuvalia tai kwa wakristo.

iii. Nguo za kuvaa ndani ya shati ambazo ni Sidiria au "vest" za rangi nyeupe au nyeusi. Haturuhusu uvaaji wa nguo zenye rangi tofauti na hizi.

iv. Tai fupi / neck tie rangi ya sketi, ziwe mbili (angalia mchoro kwenye fomu hii)

v. Waislamu waje na kanzu fupi (short kanzu) nyeupe 02, urefu wake ni hadi kwenye hipsi.Rangi ya Juba ni nyeupe kwa darasani na pinc rose kwa kushindia, ifunike kifua cha mwanafunzi, pia iwe na mikono mirefu inayofika mwanzo wa kiganja akisimama.

vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi jozi mbili.

vii. Soksi ndefu zinazofika kwenye magoti rangi ya kijivu yenye mistari miwili ya bluu na nyeupe katikati sehemu ya juu jozi mbili, na soksi nyeusi jozi moja tu.

viii. Sweta la rangi ya kijivu lililofumwa kwa uzi mzito wa kufumia.

ix. T-shirt ya shule nzito rangi moja ya kijivu aina ya manga.

### 2.2 Sare za kushindia

i. Shamba dress **(Gauni**) mbili rangi ya pink rose kwa ajili ya kushindia, urefu ni **kufunika kifundo cha miguu** kwa dini zote, kwa wenye mahitaji maalumu (wenye ualbino) shamba dress iwe na mikono mirefu **(kitambaa kizito cha suti)**

ii. Tracksuit rangi dark blue moja, yenye mistari myeupe pembeni (ambayo atavaa wakati wa kujisomea usiku).

iii. Viatu vya wazi (open shoes) kwa ajili ya kushindia jozi moja.

### 2.3 **Sare kwa ajili ya michezo**

i). Raba nyeupe jozi moja.

ii). soksi nyeupe ndefu zinazofika kwenye magoti ( stocking), jozi mbili.

iii). T-Shirt ya pink mpauko yenye kola ya duara, Isiwe na maandishi wala michoro ya rangi yoyote ile.

iv). Tight fupi nyeusi kwa ajili ya kuvalia ndani ya sketi ya michezo.

v). Sketi ya pink mpauko kitambaa cha kunguru mshono wa solo ya kuzunguka zenye ufito mweupe chini na mikanda.

**N.B Sare zote ziandikwe majina ya mwanafunzi.**






Kitambaa cha sketi ya shule


Kitambaa cha sketi ya  michezo
.(Kitambaa cha kunguru,pink mpauko)

# MISHONO WA SARE ZA SHULE

1. SKETI YA DARASANI (DRAFT)




2.





3. SHAMBA DRESS (GAUNI LA KUSHINDIA) - MBELE




SHAMBA DRESS - NYUMA



4. TIE



**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo Shuleni**

i. Picha 4 passport size akiwa amevaa shati la shule (jeupe) na ziwe na kivuli (background) ya bluu nyuma.
ii. Tranka kubwa la kutunzia vifaa vyake na Kufuri imara kwa ajili ya kufungia Tranka .
iii. Taulo (01), Vitenge au Kanga doti moja ambavyo atajifunga wakati wa kwenda kuoga
iv. Kandambili / Ndala kwa ajili ya kuogea jozi moja.
v. Godoro size ya 2.5"x 6"
vi. Shuka 3 (mbili za pinki na foronya zake na moja nyeupe na foronya yake.
vii. Mto mmoja.
viii. Chandarua 4"x6" rangi nyeupe,
ix. Blanketi 01 la kujifunika.
x. Vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe, bakuli na chupa ya chai)
xi. Pasi ya mkaa.
xii. Dumu la maji ya kunywa la lita tano – (01)
xiii. Gumboot rangi ya blue au nyeusi (buti za mpira zinazovaliwa wakati wa mvua)
xiv. Cheti cha kuzaliwa (njoo na nakala moja)

**2.3 Vifaa vya darasani.**

i. Madaftari 12 Dozen 1 (counter Book quire four (4)
ii. Madaftari 12 Dozen 1 (counter book quire two (2) kwa ajili ya mazoezi ya darasani.
iii. Boksi la kalamu za wino na penseli boksi moja la 2HB
iv. Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set).
v. Advanced Learners Dictionary.
vi. Ream paper A4 – (01) ikabidhiwe shuleni.
vii. Vitabu vya masomo vya kidato cha kwanza (vitabu vilivyochapishwa na TIE)
viii. Boksi file (faili kubwa) - (01)

**2.3 vifaa vya usafi.**

i. Ndoo tupu mbili (2) za lita 10 zenye mifuniko.
ii. Ufagio wa ndani (soft bloom) wenye mpini mrefu – (01)
iii. Mfagio wa nje ambao ni imara wa chelewa wenye mpini mrefu – (01)
iv. Brashi ngumu (hard bloom) yenye mpini mrefu kwa ajili ya kusugulia sakafu - (01)
v. Kibandizio (Squeezer) – (01)
vi. Jembe jipya lenye mpini wake- (01)
Vii. Fyekeo – (01)

NB: - ukipata changamoto yoyote ya vifaa piga simu upate maelekezo

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo, ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa ukamilifu maandalizi ya masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wako wa mwili,kutunza mavazi yako muda wote na kuhakikisha nguo zako zimekunjwa na kuwekwa vizuri kwenye tranka.
vii. Kuvaa sare za shule wakati wote kwa kuzingatia aina ya sare na wakati.
viii. Unawajibika kutunza mazingara ya shule na kufanya usafi katika maeneo yote ya shule;
ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote uwapo shuleni.
x. Kutunza mali za shule ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hakuna bomba la maji linalotiririsha maji hovyo, taa za umeme zinazimwa kwa wakati, matumizi sahihi ya vyoo vyote vya shule na utunzaji wa majengo na samani za shule.
xi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali kama kisu na dawa bila idhini ya daktari, ni marufuku kutunza vifaa vya usafi bwenini.
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa ikiwa ni pamoja na kukitunza. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu na si vinginevyo.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- ***Mwanafunzi ataruhusiwa kuja nyumbani kwa ajili ya msiba wa mama, baba, Mlezi, kaka au dada (ndugu wa tumbo moja/baba mmoja) tu na siyo ndugu mwingine. Taarifa za misiba ziletwe***

***moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule siyo kwa mwanafunzi, Mwanafunzi hataruhusiwa iwapo utaratibu huu hautafuatwa.***

- **Ni marufuku kuvaa kandambili (slipers) wakati wa chakula katika Bwalo la chakula au mazingira yoyote ndani na nje ya shule, isipokuwa bafuni wakati wa kuoga na bweni.**

- **Wageni wa mwanafunzi wanaotambulika shuleni ni wale walioandikishwa kwenye faili la mwanafunzi na wanaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi mara moja tu kwa muhula (mara 2 kwa mwaka) siku moja kabla ya mahafali ya kidato cha sita muhula wa kwanza na cha Nne muhula wa pili kwa kuitwa na Uongozi. Wasifike shuleni endapo hawajaitwa na uongozi wa shule.**

- **Likizo zote mwanafunzi atakapolazimika kwenda likizo ni sharti arudi nyumbani kwa wazazi/walezi wake, haruhusiwi kwenda kwa ndugu (Ubalozini) kipindi cha likizo fupi wala ndefu.**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugomea adhabu na kuhamasisha mgomo.
iv. Kuibia (kuangalizia) wakati wa mitihani ya ndani.
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule shuleni;
vii. Kusuka nywele, Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni(hakuna muda wa kusukana shuleni).
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa, mahusiano kati ya mwanafunzi na kijana wa kiume yanayopelekea tendo la ndoa.
xi. Kuwa mjamzito / kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kumiliki / kukutwa / kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule na ni marufuku kutumia simu ya mwalimu asiyehusika kuwasiliana nyumbani.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi mfano kuvunja kiti / meza, kupasua vioo , kuvunja milango/ makabati, madirisha nk.

***NB: hakikisha mtoto anakuja na kadi ya Bima ya Afya, kwa sababu gharama za matibabu ni kubwa sana na zinagharamiwa na Mzazi.***

***4.*** **Viambatisho na Fomu Muhimu;**

**FORM NO. 1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENTS' OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.

Pupil's full name…………………………………………………………………………

Age/Years……………………………………Sex………………………………………

Blood found (red and White)…………………………………………………………….

Stool examination:……………………………………………………………………….

Urinalysis:……………………………………………………………………………..

Venereal Diseases test:………………………………………………………………..

T.B. test:…………………………………………………………………………………

Eye Test:…………………………………………………………………………………

Ears:………………………………………………………………………………………

Chest:……………………………………………………………………………………….

Spleen:……………………………………………………………………………………

Abdomen:……………………………………………………………………………..

Urine for Pregnant:………………………………………………………………………

ADDITIONALL INFORMATION (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

………………………………………………………………………………………………..

………………………………………………………………………………………………..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: …………………………….

Designation: …………………………

Station: …… …………………………

Date: …………..……………………....

Official Stamp: ……………………….

**FORM NO. 2**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR. BATILDA BURIAN**
**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………..
2. KABILA……………………………………………………………………...
3. TAREHE YA KUZALIWA……….MWEZI…………….MWAKA………….
4. AMEZALIWA KATIKA WILAYA YA…………………………………….
   MKOA WA…………………………………………………………………..
5. DINI……………………DHEHEBU……………………………………......
6. JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………
   (Ikiwa mzazi amefariki andika jina la mlezi hapa)
7. ANWANI YA MZAZI/MLEZI:
8. S.L.P ……………………...
9. KIJIJI/MTAA ………………..
10. TARAFA …………………….
11. WILAYA/KATA …………………
12. MKOA ……………………………

Na. ya simu ya mzazi/mlezi…………………………………………….

13. KAZI YA BABA/MLEZI…………………………………………………….
14. KAZI YA MAMA/MLEZI…………………………………………………………..
15. Afya ya mwanafunzi (kama ana ugonjwa unaohitaji uangalizi uandikwe: Taja udhaifu wowote wa mwili au afya yake na uambatanishe cheti cha Daktari).
    ……………………………………………………………………………….
    ……………………………………………………………………………….
16. Majina ya Ndugu wengine wanaohusika na malezi ya huyu mwanafunzi (matatu tu), anuani zao kamili na Namba zao za simu na picha zao za passport zibandikwe kwenye maboksi mbele ya jina la ndugu.

(a) Ndugu:(Majina matatu) …………………………………………………………...
Uhusiano na Mwanafunzi:……….……………………………………………

Anwani : S.L.P …………………………………………………………..

Namba ya simu: ………………………………………………………….

(b) Ndugu:(Majina matatu) …………………………………………………………...
Uhusiano na Mwanafunzi:……….……………………………………………

Anwani : S.L.P …………………………………………………………..

Namba ya simu……………………………………………………..

(c) Ndugu:(Majina matatu) …………………………………………………………...
Uhusiano na Mwanafunzi:……….……………………………………………

Anwani : S.L.P …………………………………………………………..

Namba ya simu: ………………………………………………………….

**SAINI YA MWANAFUNZI** TAREHE

**……………………………….** **………………………..**

## FORM NO. 3

## MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi…………………………………………. (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote.

Jina laMwanafunzi ………………………………………………………….

Saini ya mwanafunzi………………………………………………………….

Tarehe……………………………………………………………………….

Shahidi(Mzazi /Mlezi)

Jina kamili………………………………………………………………………..

Saini…………………………………………………….

Tarehe……………………………………………………..

**FORM NO. 4**

## A: AHADI YA MZAZI:

Mimi ........................................................... (jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi

wa……………………………………..Kidato cha…………………. Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

Saini ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………….

Anuani kamili……………………………………………………………………….

Simu:…………………………………………

Tarehe:……………………………………….

**NB: I. Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZILIZOPO KWENYE FOMU HII.**

**II. Fomu hii ina kurasa 12 zenye maandishi, tafadhari njoo na fomu hii ikiwa na kurasa zote 12, na fomu ya hospitali ikiwa imejazwa kikamilifu.**

- **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR.BATILDA BURIAN**

……………………………………………

**MWL. CATHERINE RAPHAEL KISHIMBA**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SEKONDARI YA WASICHANA
DR.BATILDA BURIAN
S.L.P 56 KALIUA-TBR.